HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
OFISI YA RAIS TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI CHANGANYIKENI
S.L.P 1880, DAR ES SALAAM SIMU: 0714 626010
Barua pepe: changanyikeni2017@yahoo.com

Jina la mwanafunzi _____
Namba ya simu ya mzazi/mlezi:_____
Kumb. Na ……

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI

1.0 Utangulizi

Ninakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari changanyikeni kwa mwaka _____

2.0 KUFUNGUA SHULE

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza Tarehe _____ unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe _____ na mwisho wakuripoti ni tarehe_____ Ndani ya siku saba (7)

3.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Changanyikeni ipo Manispaa ya Temeke , kata ya Toangoma katika mtaa wa Mikwambe-CCM katika barabara itokayo Kongowe kwenda Kigamboni . Usafiri wa daladala unapatikana katika vituo vya Toangoma(T/Ngoma-Kigamboni),Kongowe(M/ndege-Kigamboni) na Kigamboni. Ukishuka Toangoma panda mabasi yaendayo Kigamboni shuka Mikwambe CCM ukitoka Kigamboni panda mabasi yaendayo Toangoma/Kongowe shuka Mikwambe CCM.

4.0 USAJILI

Unatakiwa kufika shuleni tarehe_____ Asubuhi saa mbili ili upate kusajiliwa na kupatiwa maendeleo kuhusu shule ukiwa na mzazi wako-mwanafunzi ataechelewa kuripoti shuleni ifikapo tarehe _____ Nafasi yake itachukuliwa na mwanfunzi wa akiba.

5.0 MOTTO WA SHULE

"**EDUCATION FOR BRIGHT FUTURE"** Elimu kwa maisha bora, Lengo kuu ni kutoa elimu inayomwezesha kijana kubadilika kitabia, kihisia na kimaono ili kukabiliana na changamoto za uhalisia wa kimaisha na kijamii.

6.0 SARE ZA SHULE KWA MSICHANA

- Sketi mbili za rangi ya kijivu iliyoiva
- Blauzi nyeupe mbili
- Soksi nyeupe mbili
- Begi la kubebea vitabu
- Hijabu na nusu kanzu
- T-shirt ya shule

- Nguo za michezo (bukta,fulana na raba)
- Tai mbili
- Singilendi nyeupe

Viatu vyeusi vya kufunga na kamba

SARE ZA SHULE KWA WAVULANA

- Suruali mbili za rangi ya kijivu iliyoiva
- Shati nyeupe mbili
- Soksi nyeusi mbili
- Begi la kubebea vitabu
- T-shirt ya shule
- Nguo za michezo (bukta,fulana na raba)
- Tai mbili
- Singilendi nyeupe
- Mkanda mweusi wenye kifungo cha kawaida cha kawaida

Viatu vyeusi vya kufunga na kamba

VIFAA VINGINE

I. Mkebe mmoja(Mathematical set)
II. Peni, Rula, penseli
III. Mathematical table(Four Figure)
IV. Madaftari kumi na mbili (Aina ya Professor au counter book)
V. Students Dictionary(Oxford)
VI. Vitabu vya darasani angalau masomo manne

7.0 MENGINEYO MUHIMU

8.0 Matumizi na mahitaji ya mwanafunzi yanakutegemea zaidi wewe mzazi/mlezi. Ni imani yetu utampatia mwanao kila aina ya msaada ili aweze kusoma kwa umakini. **SIMU YA MKONONI NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI**

9.0 MWISHO

Uongozi wa shule unawatakia maandalizi mema ya kujiunga na shule yetu. Ni matumaini yetu utazingatia kanuni na sheria za shule ili lengo lililokuleta shuleni liweze kukamilika. Kauli yetu kwa pamoja “ELIMU KWA MAISHA BORA”

……

Mkuu wa shule
Shule ya sekondari changanyikeni
S.L. P 1880
Dar es salaam

NAKALA KWA:-

1. Mkaguzi wa shule
   Kanda ya Dar es salaam
   S.L.P 9403
   Dar es salaam
2. Afisa Elimu (M)
   Mkoa wa Dar es salaam

S.L.P 5429
Dar es salaam

3. Afisa Elimu Sekondari (W)
   Mkoa wa Dar es salaam
   S.L.P 46343
   Dar es salaam
4. Afisa Elimu kata Sekondari
   Mkoa wa Dar es salaam
   S.L.P 46343
   Dar es salaam

SHERIA ZA SHULE

A. MAHUDHURIO

1. Kila mwanafunzi ni lazima afike shuleni asubuhi saa moja kamili(1:00) na kufanya usafi wa mazingira na kuhudhuria gwaride na ukaguzi wa usafi wa kuchangamsha mwili
2. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali/ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa darasa, mwalimu wa zamu na mkuu wa shule
3. Mwanafunzi haruhusiwi kutohudhiria shuleni bila kupata kibali. Ruhusa itatolewa kwa sababu maalum tu kwa ombi la mzazi/mlezi. Mwanafunzi akikosa zaidi ya siku tatu mfululizo atalazimika kufika pamoja na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni.
4. Mwanafunzi ni **LAZIMA** afanye mitihani ya masomo yote aliyojiandikisha shule ambayo imeandaliwa shule au kutoka nje ya shule.

B. VAZI RASMI LA SHULE

Kila mwanafunzi analazimika kuvaa na kuheshimu vazi rasmi(uniform) la shule wakati wote anapokuwa katika eneo la shule au nje ya shule kwa shughuli rasmi za shule. Siku ya Ijumaa na siku za michezo wanafunzi wavae Tshirt za shule.

C. VITU VISIVYORUHUSIWA

1. Kuvaa pete
2. Kuvaa herein
3. Kupaka hina
4. Kucha ndefu
5. Kusuka Nywele
6. Kukali au kulilax ni marufuku
7. Kunyoa nyusi
8. Hairuhusiwi kunyoa mitindo
9. Hairuhusiwi kunyoa vipara
10. Hairuhusiwi kuvaa mabuti na viatu vinavyofanana na vya jeshi
11. Hairuhusiwi kuvaa sandozi, mikanda isiyoendana na vazi rasmi la shule
12. Mashati makubwa sana na slim fit hayaruhusiwi.

D. MALI YA SHULE

1. Mwanafunzi akikabidhiwa vifaa kama vitabu vya kusomea anatakiwa kuviangalia sana na sharti avirudishe kwa mwalimu aliyemkabidhi kila vinapohitajika kurudishwa.

2. Ieleweke kwamba ni kosa kubwa sana kuharibu mali yoyote ya shule ikiwa ni pamoja na majengo. NI MARUFUKU KUPIGA MACHATA katika ukuta au majengo. Adhabu yake ni kufukuzwa shule.
3. Kifaa chochote kitakachopotea sharti kilipwe. Cheti cha kumaliza shule hakitatolewa kwa yeyote ambaye hatarudisha au kulipa vifaa alivyopoteza au kuharibu.
4. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa nabegi la kuhifadhi vitabu vyake. HAIRUKUSIWI KUBEBA VITABU VYAKO MKONONI.

E. KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule ipo kwa ajili ya kutoa Elimu. Kama ilivyo katika jamii yeyote yenye lengo maalimu ni lazima shule iwe na sheria au taratibu zitakazowezesha jamii ya shule kutekeleza majukumu yake. Sheria ni taratibu hizo ni lazima ziwekwe wazi na zieleweke na kila mmoja na zifuatwe kikamilifu.
Zifuatazo ni kanuni au taratibu zinazohusu wanafunzi wa shule ya sekondari changanyikeni zenye lengo la kuweka mazingira ya ufanisi kazi namalezi hapa shuleni kulingana na matakwa ya Taifa letu la Tanzania.

1. NIDHAMU NA MWENENDO

a. Kila mwanafunzi lazima awe na nidhamu ya hali ya juu kuheshimu wafanyakazi wote na wanajumuiya kwa ujumla , Mwanafunzi asiye na nidhamu atapoteza nafasi yake Usimpige au kumshambulia mwanafunzi mwenzako ama ata mtu mwingine yeyote

b. Usikatae uteuzi kushiriki shughuli mbalimbali kama vile michezo, maandamano uwakilishi n.k

c. Usigune wala kuzomea wakati mwalimu au kiongozi yeyote anapotoa matangazo.

d. Usibandike tangazo lolote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.

e. Hotuba zote lazima zionwe na mkuu wa shule, kabla ya kutolewa katika hadhara yoyote shuleni.

f. Usifanye mkutano bila ya ruhusa ya mwalimu anaye husika kukilea kikundi kinachohusika.

g. Usihubiri dini,siasa au jambo lolote sala zote zianyike mahali panapo husika kama vile kanisani au msikitini.

a. Baadhi ya makosa ya utovu wa nidhamu ni:-
   I. Uchelewaji kwenye gwaride
   II. Kutofanya kazi za usafi wa mazingira
   III. Kutojali masomo na uzalishaji mali
   IV. Dharau,ukaidi,ubishi,utoro,uvivu,wizi,ulevi,upigaji kelele.
   V. Kunyoa mitindo/upara
   VI. Makosa kama uasherati, uvutaji bangi/madawa ya kulevya, kukashifu viongozi na kudharau bendera ya Taifa ni makosa ambayo husababisha mwanafunzi kufukuzwa shule bila kuonywa. Mwanfunzi anazo nafasi mbili tu za kuonywa na baada ya hapo kikao cha bodi ya shule kitamchukulia hatua kali zaidi.
   VII. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.

VIII. Kugoma na kuhamasisha mgomo.

IX. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujuma.

X. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, Kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

XI. Kufuga ndevu.

XII. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

XIII. Uvutaji wa sigara.

XIV. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

XV. Kupata ujauzito au kutoa ujauzito.

XVI. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

XVII. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

XVIII. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

XIX. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

2. SHERIA YA JUMLA

Kila wakati fikiria kwanza kabla ya kunena na tumia busara kutenda

3. ADHABU

- Adhabu zitaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi anaye onesha utovu wa nidhamu.
- Kiranja pia anaruhusiwa kutoa adhabu kulingana na kosa lililotendwa na mwanafunzi ilimradi asipige kiboko au kuzuia kuingia darasani wakati wa masomo.
- Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jalada la mwanafunzi na kitabu cha kumbukumbu za adhabu.

FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)

A: IJAZWE NA MWANAFUNZI:

PICHA YA MWANAFUNZI

- Jina kamili la mwanafunzi……....
- Taifa……
- Uraia……..
- Dini……..
- Tarehe ya kuzaliwa……

- Mahali alipozaliwa…… Wilaya……
- Shule aliyosoma kabla ya kuja shule ya sekondari

  ……

Shule ya msingi	Tarehe na mwaka aliomaliza	Tarehe na mwaka aliotoka
I		
II		
III		
IV		

8. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

9. Saini ya mwanafunzi ……..

PICHA YA MZAZI/MLEZI

B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI:

- Jina kamili……..
- Utaifa …… ……
- Uraia……
- Anuani kamili mjini Dar es salaam……
- Sehemu unayoishi……... Picha ya Mzazi/Mlezi
- Mtaa……..
- Namba ya nyumba…….
- Simu ya mkononi: Baba/mlezi…….. Mama/ Mlezi……

C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/ MLEZI:

- Jina la mwajiri na Idara…….
- Kazi ya mzazi/ Mlezi (Meneja, Daktari, Mfanyabiashara n.k)……..

D: SOMO LA DINI

Mimi……ambaye ni Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....Kidato cha…… Ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la dini ya …… Dhehebu la ……. Siku ya ALHAMISI akiwa shuleni Changanyikeni sekondari.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……